Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 2 Issue 1 | [December] [2025] | [Page 230] – [Page 246]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

# Uashiriaji Wa Kijinsia Kama Suala Mahususi La Kitamaduni: Mchango Wa Uashiriaji Wa Kijinsia Katika Mwachano Wa Maana Kwenye Tafsiri Za Nyimbo

Edward Mariga
Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga

Corresponding author: marigaedward@gmail.com

**Article History:**
**Received:** 30 Sept 2024
**Accepted:** 13 June 2025
**Published:** 26 Dec 2025

**Maneno muhimu:**
Tafsiri, Jinsia ya Kisemantiki, Jinsia ya Kisarufi, Nadharia ya Wingimifumo na Masuala Mahususi ya Kitamaduni

*This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license*

**Ikisiri**

Makala haya yanachunguza jinsia kama suala mahususi la kitamaduni katika tafsiri zinazofanywa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili na kwa msingi huo kubaini nafasi ya uashiriaji wa kijinsia katika mwachano wa maana katika tafsiri za aiana hiyo. Suala mahususi la kitamaduni likimaanisha suala linalopatikana katika lugha moja na kukosekana katika lugha ya pili katika tafsiri. Utafiti ulichochewa na mwelekeo wa tafiti za awali kuwa tofauti za maana katika tafsiri ni matokeo ya upungufu katika tafsiri. Utafiti huu ulichukua mwelekeo kuwa si tofauti zote za maana katika tafsiri ni ishara ya uchapwa katika tafsiri husika. Matini zilizochunguzwa katika utafiti huu ni pamoja na 'Nyimbo za Kristo' kama matini lengwa na matini chasili 'The Seventh Day Adventist Hymnal' ambapo data zilikusanywa kwa njia ya uchanganuzi matini. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya wingimifimo ya Gideon Touri (1980). Utafiti huu ulihusu eneo la fasihi tafsiri ambapo usampulishaji dhamirifu ulitumika. Kati ya nyimbo 220 katika matini lengwa zilizochunguzwa, 116 zinazodhihirisha masuala ya kijinsia zilifanyiwa uchanganuzi linganuzi ili kubaini masuala ya kitafsiri yaliyoibuka kuhusu jinsia. Matokeao ya utafiti yalionyesha kuwa jinsia ni suala mahususi katika tafsiri zinazofanywa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili na hivyo kuchangia mwachano wa maana. Aidha, utafiti ulionyesha kuwa tofauti za maana kati ya matini mbili husika zilizohusishwa na masuala ya kijinsia, hazikutokana na upungufu wa kitafsiri bali tofauti katika uashiriaji wa kijinsia kati ya lugha mbili husika.

**Abstarct**

This article investigated gender as a culture-specific item in translations done from English to Kiswahili focusing on its role in causing differences in meaning in song translation. In translation, a culture-specific item refers to a concept or term that exists in one language but has no direct equivalent in the second. This research was motivated by previous studies which opined that differences in meaning in translation often imply poor translation. However, this study argues that not every difference in meaning results from translation inadequecies. The texts analyzed included Nyimbo za Kristo as the target text and The Seventh Day Adventist Hymnal as the source text. Gideon Toury's Polysystemic theory (1980) was used in this study as the theoretical framework. Purposive sampling was used within the domain of translated literature. Out of 220 hymns in the target text, 116 containing gender markers were comparatively analyzed to identify gender related translation issues. The research findinds revealed that gender functions as a culture-specific item in translations done from English to Kiswahili and greatly contributes to sematic shifts. Additionally, the meaning differences observed in the study were attributed not to poor translation practices but to differences in gender marking between the two languages in the study.

**Keywords:** Translation, Semantic Gender, Grammatical Gender, Polysystemic Theory

## 1.0 Utangulizi

Lugha mbili zinapotangamana katika muktadha wa kitafsiri, panaweza kuibuka vipengele fulani vya lugha vinavyopatikana katika lugha chasili na kukosekana katika lugha lengwa. Hali kama hii ambapo vipengele fulani vinadhihirisha umahususi katika lugha fulani (vinapatikana katika moja lakini haviko katika lugha nyingine) kati ya lugha mbili zinazohusika katika tafsiri, huweza kuibua hali ambapo maana katika matini chanzi na matini lengwa zinatofautiana. Miongoni mwa vipengele hivi ni kipengele cha jinsia. Yaani, ikiwa lugha mbili zinazohusika katika tafsiri zinatofautiana katika jinsi ya kuashiria jinsia basi maana kati ya matini chasili na matini lengwa huweza kutofautiana. Ni katika msingi huu ambapo makala haya yalichunguza jinsi ambavyo tofauti katika uashiriaji wa kijinsia kati ya lugha ya Kiingereza na ile ya Kiswahili zinavyochangia tofauti za maana katika tafsiri za nyimbo kwa kurejelea matini mbili zilizohusishwa kwenye utafiti huu.

Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa kuna jinsia ya aina mbili; jinsia ya kisarufi na jinsia ya kibayolojia. Wanasema kuwa lugha huambiwa kuwa na jinsia ya kisarufi ikiwa maneno yake yanatiwa katika makundi ya uana bila kuzingatia sifa za kibayolojia. Kwa mfano wanasema kuwa katika Kifaransa gari dogo liko katika jinsia ya kike na lori iko katika jinsia ya kiume. Wanaeleza kuwa Kiswahili hakidhihirishi mahusiano haya ya kijinsia kiupatanisho bali hutumia nomino zinazorejelea jinsia kama vile Sabina, Omari, mama, baba, mjomba na shangazi. Maelezo haya ya Habwe na Karanja yanabainisha kuwa lugha ya

Kiswahili inakosa uashiriaji wa jinsia kisarufi. Kwa msingi huu, ikiwa matini ya Kiingereza inayotafsiriwa kwa Kiswahili imetumia jinsia ya kisarufi basi maana huweza kuwa tofauti.

## 2.0 Msingi wa Nadharia

Nadharia hii iliasisiwa na Itamar Even-Zohar mwanzoni mwa miaka ya sabini na kuboreshwa na Gideon Toury (1980). Kimsingi, nadharia hii inatoa mwelekeo wa kuchunguza kazi ya fasihi tafsiri sambamba na kani za kitamaduni, kihistoria na kijamii za lugha lengwa. Aidha, nadharia hii inadai kuwa uchunguzi wa matini iliyotafsiriwa unastahili kufanywa katika muktadha wa mifumo ya kitamaduni na kifasihi ya lugha lengwa.

Nadharia za awali za tafsiri zilijaribu kubaini ubora wa tafsiri kwa misingi ya kufanana kimaana kwa matini lengwa na matini chanzi. Mwelekeo huu ulionekana kutukuza lugha chanzi huku ukidunisha au kutoipa uzito lugha lengwa. Mtazamo huu ulichukulia tafsiri kama chakato wa kiisimu pekee na kupuuza masuala muhimu kama vile miktadha ya kitamaduni. Mwelekeo huu ulipingwa sana na Toury. Aliiona fasihi kama mfumo mkuu ulio na mitandao ya mifumo midogo ndani yake inayotegemeana na kuathiriana. Hivi ni kumaanisha kuwa, mifumo ya kiisimu na ya kitamaduni ya lugha zinazohusika katika tafsiri ni mifumo inayoshawishi uibukaji wa matini tafsiri. Katika kuathiriana huku kwa mifumo hii ya kiisimu na ya kitamaduni, maana kati ya matini chanzi huweza kutofautiana hususan pale ambapo suala fulani linapatika katika utamaduni wa lugha chanzi na kukosekana katika utamaduni wa lugha lengwa.

Yaani, Toury alishikilia kuwa lugha mbili zinapotagusana katika miktadha ya tafsiri, panaibuka masuala yanayodhihirisha umahususi katika utamaduni wa lugha mojawapo kati ya zile mbili zinazohusika katika tafsiri. Masuala haya yanarejelewa kama masuala mahususi ya kitamaduni. Hii ndiyo sababu Toury alidai kuwa hakuna tafsiri ambayo inaweza kufanana kikamilifu na lugha chanzi kwani tafsiri ni sharti iongozwe na kaida mbalimbali za kitamaduni ambazo zina umuhimu katika kushawishi tafsiri. Hivi ni kumaanisha kuwa vipengee vya kitamaduni kama vile jinsia vinaweza kubaini jinsi tafsiri inavyofanywa katika lugha lengwa. Kwa msingi huu, utafiti huu basi unaona tofauti katika uashiriaji wa kijinsia kati ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili kama ni kipengele kimojawapo cha kitamaduni kinachochangia mwachano wa maana katika tafsiri za nyimbo.

## 3.0 Udhihirikaji wa Jinsia katika Tafsiri

Jinsia hurejelea uanishaji wa kibayolojia au wa kijamii wa kitu au kiumbe kuwa ni wa kike au a kiume. Kwa mujibu wa Habwe na Zaja (2019) jinsia au uana ni uainisho katika lugha unaoonyesha hali ya kike, kiume au uhoromo – yaani nomino isiyo na jinsia. Maelezo haya ya Habwe na Zaja yanaashiria kuwa jinsia hufungamana na lugha husika na mfumo wa kitamaduni wa lugha husika. Hii ni kwa sababu lugha mbalimbali huashiria masuala tofauti

ya kijinsia kwa namna mbalimbali na inayotofautiana kutoka lugha moja hadi nyingine. Jinsia huweza kugawika katika makundi mbalimbali. Kwa mfano, kwa mujibu wa Stitt R. (2016) jinsia huweza kugawika katika jinsia ya kiisimu, jinsia ya kisemantiki na jinsia ya kijamii. Migao hii ya jinsia huashiria masuala mbalimbali ambayo yanapohusishwa katika tafsiri huweza kuibua masuala mbalimbali ya kitafsiri. Katika utafiti huu, jinsia zilizoibuka katika matini zilizochunguzwa na ambazo zilijadiliwa ni jinsia ya kisemantiki pamoja na jinsia ya kisarufi.

### 3.1 Jinsia ya Kisemantiki

Jinsia ya kisemantiki hutaja viumbe kuwa wa kike, wa kiume, au bila jinsia kwa misingi ya kibayolojia. Katika nyimbo za kidini zilizochunguzwa, jinsia ya kisemantiki imejitokeza kupitia viwakilishi, nomino na virai nomino.

#### 3.1.1 Viwakilishi

Matei (2014) anaeleza kuwa viwakilishi hutumika badala ya nomino na vinaweza kudokeza jinsia. Katika tafsiri za nyimbo, viwakilishi vinavyobeba jinsia katika Kiingereza hupoteza dhana hiyo katika Kiswahili. Viwakilishi vilivyojitokeza katika matini chanzi pamoja na tafsiri zao katika matini lengwa ni kama vifuatavyo:

**Kiwakilishi ‘he’**

Katika nyimbo 116 kwenye matini lengwa yaliyoashiria jinsia katika matini chanzi, kiwakilishi hiki kimetumika mara 172. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hiyo:

> **To God be the Glory**
>
> Great things **he** hath taught us, great things he hath done, and great our rejoicing thru Jesus the Son; but purer, and higher, and greater will be our wonder, our transport, when Jesus we see - **A**litufundisha mambo makuu, Alihakikisha wokovu wetu; Lakini zaidi ajabu kubwa, Yesu atakuja na tutamwona.
>
> **I will sing of jesus' love**
>
> I Will sing of Jesus love, Sing of Him,who first loved me; for **He** left bright worlds above, And died on Calvary. - Niimbe (niimbe) pendo lake, pendo la (pendo la) Yesu Bwana; Sababu (sababu) **a**litoka Kwa Baba akafa.

Katika mifano hii, kiwakilishi **‘he’** katika matini chasili huwakilisha jinsia maalumu; yaani jinsia ya kiume. Hata hivyo, katika matini lengwa, kiwakilishi hiki kimechukua kiambishi

**'a'** ambacho hakidokezi jinsia maalumu. Hali hii ya dhana fulani kuhusishwa na jinsia maalumu katika matini chasili lakini uashiriaji huo wa kijinsia kupotea katika matini lengwa inachangia katika tofauti za maana matini hizi mbili zikilinganishwa. Maelezo kuhusu tofauti hizi kwa mujibu wa nadharia ya wingimifumo ni kwamba lugha ya Kiingereza kama lugha chasili inaashiria jinsia ya kiume kwa kutumia kiwakilishi **'he'** jambo ambalo linakosekana katika lugha ya Kiswahili kama lugha lengwa. Kwa msingi huu basi, maana katika tafsiri za nyimbo kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili huweza kutofautiana kwa sababu lugha ya Kiingereza huashiria jinsia kwa njia inayotofautiana na lugha ya Kiswahili.

**Kiwakilishi 'him'**

Kiwakilishi kimetumika mara 157 katika nyimbo 116 zilizoashiria jinsia katika matini chasili. Ifuatayo ni baadhi ya mifano:

> **<u>Heir of the kingdom</u>**
>
> Heir of the kingdom, say, why dost thou linger? How canst thou tarry in sight of the prize? Up, and adorn thee, the Saviour is coming; Haste to receive **Him** descending - Mrithi ufalme mbona 'kawia'? M-bona hupokei zawadi? Haya uvae, Mwokozi yuaja; Haraka, u**m**laki apitapo.
>
> **<u>My lord and I</u>**
>
> I tell **Him** all my sorrows, I tell Him all my joys, I tell Him all that pleases me, I tell Him what annoys; He tells me what I ought to do, He tells me how to try, And so we talk together, My Lord and I. - Na**m**weleza huzuni na furaha yangu, Vile vinavyosumbua Vinavyopendeza; Huniagiza kutenda Yanayonipasa Twazungumza pamoja Bwana nami.

Katika mifano ya hapo juu, inadhihirika kuwa kiwakilishi '**him**' katika matini chasili ambacho kinahusishwa na jinsia ya kiume kimetafsiriwa katika matini legwa kupitia kiambishi '**m**'. Hali hii inafanya maana iliyopo katika matini chasili na maana katika matini lengwa kuhusu dhana husika kutofautiana. Hivi ni kumaanisha kuwa nyimbo zinapotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili, maana katika mtini chasili huweza kutofautiana na maana katika matini lengwa kwa sababu lugha ya Kiingereza huashiria jinsia mahususi (ya kiume) kupitia kwa kiwakilishi '**him**' tofauti na lugha ya Kiswahili ambayo inatumia kiambishi '**m**' ambacho hakihusishwi na jinsia yoyote.

**Kiwakilishi 'his'**

Kiwakilishi hiki kimetumika mara 358 katika nyimbo 116 zilizoashiria jinsia katika matini

chasili. Beti zifuatazo ni baadhi ya mifano inayodhihirisha kiwakilish hiki.

**I've found a Friend**

I've found a Friend, oh, such a Friend! So kind, and true, and tender, So wise a counsellor and guide So mighty a defender. From Him, who loveth me so well; What power my soul can sever? Shall life or death, or earth, or hell? No; I am **His** forever. - Ninaye Rafiki naye Yuna na moyo mwema, Ni Mwalimu Kiongozi, Mlinzi wa daima; Ni nani wa kunitenga, Na mpenzi wa mbele? Kwake nimetia nanga, Ndimi **wake** milele.

**Tis Love that Makes us Happy**

God is love; we're **His** little children. God is love, we would be like Him. 'Tis love that makes us happy, 'Tis love that smooths the way; It helps us "mind," it makes us kind To others every day - Yu Pendo: Tu Watoto **Wake**. Yu Pendo, Mwana Wa Mungu! Na Sisi Tupendane Kama Baba Mungu. Amri Yake Ndiyo Hii, Kupendana Sana.

Katika mifano hii, kiwakilishi '**his**' katika matini chasili ambacho kinaashiria jinsia ya kiume, kimetafsirirwa kuwa '**wake**' katika matini lengwa. Mfano huu pia unadhihirisha hali ambapo matini chasili inatofautiana kimaana na matini lengwa kwa sababu lugha ya Kiingereza huashiria jinsia kwa njia tofauti na lugha ya Kiswahili.

### 3.1.2 Virai Nomino

Kirai hurejela fungu la maneno ambalo halina muundo wa kiima na kiarifu na ambalo hufanya kazi kama neno moja. Kulingana na Matei (2014), kirai nomino ni aina ya kirai ambacho kichwa chake ni nomino au kiwakilishi cha nomino na ambacho hufanya kazi kama nomino. Virai hivi katika matini chasili pia vinadhihirisha jinsia maalum. Hata hivyo, katika matini lengwa, uashiriaji huo wa jinsia maalum unakosekana kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

**To God be the Glory**

To God be the glory, great things he hath done! So loved he the world that he gave us his Son, who yielded **his life** an atonement for sin, and opened the lifegate that all may go in. - Mungu atukuzwe, kwa mambo makuu, Upendo wake ulitupa yesu, Aliyejitoa **maisha yake**, Tuwe nao uzima wa milele.

**I will sing of Jesus Love**

I will sing of Jesus love Endless praise my heart shall give; He has died that I might live I will sing **His love** to me. - Niimbe (niimbe) pendo lake; Sifa kuu (sifa kuu) nitatoa; Akafa (akafa) niwe hai, Niimbe **pendo lake**.

**Redeemed how I love to proclaim it**

Redeemed! how I love to proclaim it Redeemed by the blood of the Lamb; Redeemed through His infinite mercy, **His child**, and forever, I am. - Nimekombolewa na Yesu na sasa nimefurahi; Kwa bei ya mauti yake mimi ni **mtoto wake**.

Mifano ya hapo juu ni mifano ambapo kirai nomino kinaundwa kwa nomino na kivumishi katika matini chasili. Katika mifano hii, tafsiri zake katika matini lengwa pia imefanywa ikiwa na nomino na kivumishi chake. Hata hivyo, uashiriaji ya jinsia ya kiume ambao unadhihirika katika matini chasili unakosekana katika matini lengwa. Mifano mingine ya virai nomino vinavyoashiria jinsia katika matini chanzi kwenye nyimbo zilizochunguzwa ni kama ifuatavyo:

His life – maisha yake

His love – pendo lake

His child – mtoto wake, mwana wake

His beauty – uzuri wake

His blood – damu yake

His love – wema wake

His word – neno lake

His feet – miguuni pake

His children – watoto wake

His righteousness – haki yake

His appearing - kuja kwake

His glory – utukufu wake

His presence – mbele yake

Katika mifano yote hii, maana inayotokana na jinsia katika matini chanzi inapotea katika matini lengwa. Tofauti hizi za maana zinatokana na uhalisia kuwa lugha ya Kiingereza inadhihirisha umilikaji unaohusishwa na jinsia fulani katika virai nomino ilhali lugha ya Kiswahili haina uashiriaji huu wa kijinsia. Hata hivyo, kunadhihirika pia hali ambapo virai nomino vinavyoundwa kwa nomino pamoja na vivumishi viwili katika matini chasili vikihawilishwa hadi matini lengwa, kivumishi kimoja kinadondoshwa. Udondoshaji huu unatokana na hitaji la kupata idadi inayohitajika ya silabi ili kufanikisha uimbikaji. Pamoja na udondoshi huo, maana inayoekezwa na jinsia ya kiume katika matini chasili inakosa kudhihirika katika matini lengwa. Tazama mifano ifuatayo

**Come thou fount**

Here I raise mine Ebenezer; hither by thy help I'm come; and I hope, by thy good pleasure, safely to arrive at home. Jesus sought me when a stranger, wandering from the fold of God; he, to rescue me from danger, interposed **his precious blood**. - Namshukuru sana Bwana, aniwezesha huku. Salama aniongoza hata kule nyumbani. Yesu alinitafuta njiani mbali kwake, Akatoa **damu yake** nipone hatarini.

**Crown Him**

Crown Him the Lord of peace! Whose hand a sceptre sways From pole to pole, that wars may cease, And all be prayer and praise; His reign shall know no end, And round **His pierced feet**

Fair flowers of Paradise extend, Their fragrance ever sweet. - Taji mvikeni Bwana wa Mapenzi; **Jeraha zake** ni shani Ni vito vya enzi, Mbingu haina Hata malaika Awezae kuziona pasipo kushangaa!

Katika kundi hili la virai nomino, imetafsiriwa kama ifuatavyo:

His precious blood – damu yake

His pierced feet – jeraha zake

His infinite mercy – mauti yake

His wondrous love – pendo lake

His excellent word – neno lake

His clansing blood – damu yake

His faithfull and happy children – watu wake

His loving care – ulinzi wake

His father's bright glory – fahari ya baba yake

His little children – watoto wake

His loved ones – wateule wake

Pamoja na udondoshaji unaodhihirika katika mifano hii, kuna pale ambapo mtafsiri amefanya tafsiri fasiri. Kwa mfano ‘his pierced feet – jeraha zake’, ‘infinite mercy – mauti yake’ na ‘his loved ones – wateule wake’. Hata hivyo, udondoshi huu pamoja na tafsiri iliyofanywa kwa njia ya kiufasiri ni mbinu ambazo zimetumika kufanikisha idadi maalumu ya silabi ili kudumisha uimbikaji wa nyimbo husika. Kuhusu jinsia, inabainika wazi wa jinsia inayohusishwa na virai hivi katika matini chasili inakosa kudhihirika katika matini lengwa.

Aidha, kuna pale ambapo virai nomino husika vimeundwa kwa nomino na vivumishi viwili na uhawilishaji wake umefanywa kikamilifu bila udondoshaji. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hii.

**When the trumpet of the Lord shall sound**

Let us labor for the Master from the dawn till setting sun, Let us talk of all **His wondrous love** and care, Then, when all of life is over, and our work on earth is done, And the roll is called up yonder I'll be there - Tutende kazi kwa yesu mchana kutwa kwa bidii, Tutangaze kote **pendo lake kuu**, Nayo kazi itakapotimika hapa chini Majina yaitwapo, lo! niweko.

**More about Jesus**

More about Jesus, I would know, More of His grace to others show; More of **His saving fullness** see, More of His love who died for me. - Nataka nimjue Yesu, na nizidi kumfahamu, Nijue pendo lake tu, **wokovu wake kamili**.

Katika mifano hii, bado maana inayojitokeza katika matini asilia kutokana na dhana za kijinsia zinapotea katika matini lengwa.

### 3.1.3 Nomino

Waihiga (1999) anafasiri nomino kama neno linalotaja mtu, kitu, hali au mahali. Maelezo haya ya Waihiga yanawiana na maelezo ya Matei (2014) ambaye anasema kuwa nomino ni neno linalotaja mtu, hali, kitu na maeneo. Katika matini chanzi, zipo nomino zilizotumika na ambazo zinadhihirisha jinsia maalum. Nomino hizi ni kama vile ‘father’, ‘son’, ‘king’ na ‘bridegroom’. Katika utafiti huu tafsiri za nomino zilidhihirika kama ifuatavyo:

**Father**

Katika matini chanzi, nomino hii imetumika mara kumi na saba. Katika mara zote hizo, neno hili linaashiria jinsia ya kiume (mzazi wa kiume). Katika matini lengwa, nomino hii imetafsiriwa kama baba (mzazi wa kiume), neno ambalo pia linaashiria jinsia ya kiume inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

**To God be the Glory**

Praise the Lord, praise the Lord, let the earth hear his voice! Praise the Lord, praise the Lord, let the people rejoice! O come to the **Father** thru Jesus the Son**,** and give him the glory, great things he hath done! - Msifu, msifu dunia sikia; Msifu, msifu, watu wafurahi; Na uje kwa **baba**, kwa yesu mwana Ukamtukuze kwa mambo yote.

**Praise god from whom all blessings flow**

Praise God from whom all blessings flow; Praise Him all creatures here below; Praise Him above ye heavenly host; Praise **Father,** Son and Holy Ghost. Amen - Msifu Mungu wa neema, Enyi viumbe po pote; Wa juu pia sifuni **Baba**, Mwana naye Roho!

Katika mifano yote hiyo, tafsiri ya nomino hii katika matini lengwa inaibua hali ya ulinganifu wa maana kati ya matini mbili husika. Ulinganifu huu unatokana na hali kwamba lugha chanzi na lugha lengwa zinaashiria jinsia kupitia kwa nomino husika.

**Son**

Nomino hii katika matini chanzi imetumika mara nane. Katika mara zote hizo, nomino hii inaashiria jinsia ahususi (mwana wa kiume). Hata hivyo, katika matini lengwa, nomino hii imetafsiriwa kama mwana, nomino ambayo haiashirii jinsia yoyote kama ilivyo katika mifano hii:

**To God be the Glory**

Praise the Lord, praise the Lord, let the earth hear his voice! Praise the Lord, praise the Lord, let the people rejoice! O come to the Father thru Jesus the **Son,** and give him the glory, great things he hath done! - Msifu, msifu dunia sikia; Msifu, msifu, watu wafurahi; Na uje kwa baba, kwa yesu **mwana** Ukamtukuze kwa mambo yote.

**Praise god from whom all blessings flow**

Praise God from whom all blessings flow; Praise Him all creatures here below; Praise Him above ye heavenly host; Praise Father, **Son** and Holy Ghost. Amen -

> Msifu Mungu wa neema, Enyi viumbe po pote; Wa juu pia sifuni Baba, **Mwana** naye Roho!

Hali hii husababisha maana kati ya matini chasili na maana katika matini lengwa kutofautiana. Tofauti hii inatokana na lugha ya Kiingereza na lugha ya Kiswahili kuashiria jinsia kwa njia tofauti kupitia nomino inayotaja mtoto wa kiume.

**King**

Nomino 'king' inaashiria jinsia ya kiume (kiongozi wa kiume). Katika matini chanzi, nomino hii imetumika mara kumi na tisa. Katika matini lengwa, nomino hii imetafsiriwa kama mfalme au bwana. Tafsiri bora zaidi kwa neno 'king' ni mfalme na hii ndiyo tafsiri iliyotumika sana. Hata hivyo, kunayo mifano ambapo katika matini lengwa, mtafsiri ametumia neno bwana ambalo katika lugha ya Kiingereza ni tafsiri ya neno 'Lord' kama ilivyo katika mfano ufuatao:

> **Nearer, still nearer**
>
> Nearer, still nearer, nothing I bring, Nought as an offering to Jesus my **King** Only my sinful now contrite heart; Grant me the cleansing Thy blood doth impart, Grant me the cleansing Thy blood doth impart. - Karibu sana, sina kitu sina, Sadaka kwa **Bwana** Yesu, Isipokuwa moyo wangu: Uutakase katika damu, Uutakase katika damu.
>
> **Redeemed how i love to proclaim it**
>
> I know I shall see in His beauty The **King** in whose law I delight Who lovingly guardeth my footsteps And giveth me songs in the night - Nitamwona **mfalme** wangu katika uzuri wake, Ambaye najifurahisha katika torati yake.

Katika mikondo hii miwili ya kutafsiri neno 'king', maneno bwana na mfalme yanadhihirisha jinsia ya kiume katika matini lengwa. Hata hivyo, ulinganifu wa maana unajitokeza pale ambao mtafsiri ametumia neno mfalme katika matini lengwa. Hali hii inatokana na kuwepo kwa uashiriaji sawa wa kijinsia kupitia nomino husika kati ya lugha hizi mbili. Pale ambapo mtafsiri ametumia neno bwana, mwachano wa maana katika ya lugha chanzi na lugha lengwa unajitokeza. Hali hii imesababishwa na mtafsiri kutaka kufanikisha uimbikaji kwa kudumisha idadi mahususi ya silabi kwenye mshororo husika.

**Bridegroom**

Nomino ‘bridegroom’ inaashiria jinsia ya kiume. Nomino hii imetumika mara sita katika matini chanzi na katika mara zote hizo, tafsiri yake ni bwana wa arusi. Tafsiri hii, sawa na matini lengwa inadhihirisha jinsia ya kiume kama ilivyo katika mfano ufuatao:

> **The golden morning**
>
> The gospel summons will soon be carried To the nations round The **Bridegroom** then will cease to tarry And the trumpet sound - Injili inatangazwa pote kwa mataifa**;** **Bwana wa Arusi** atakuja Na tarumbeta.

Hali hii ya ulinganifu wa maana inatokana na uhalisia kuwa lugha mbili husika zinaashiria jinsia kupitia kwa nomino husika.

**3.1.4 Jinsia Moja Kusimamia Jinsia zote**

Katika Kiingereza, baadhi ya nomino hutumika kusimamia jinsia zote mbili, lakini katika Kiswahili tafsiri yake inakosa uashiriaji wa jinsia. Nomino hizi ni pamoja na ‘watchman’ au ‘watchmen’ pamoja na ‘men’ inavyodhihirika katika mifano ifuatayo;

**Watchmen au watchmen**

Nomino hizi zimetumika mara kumi na nne katika matini chanzi. Katika mara zote hizi, nomino hii inaashiria jinsia ya kiume na jinsia ya kike. Katika matini chanzi, nomino hizi zimetumika kuashiria jinsia zote; jinsia ya kiume na ya kike. Katika matini lengwa, nomino hizi zimetafsiriwa kama mlinzi, walinzi au mkesha kama inavyodhihirika katika mifano hii:

> **Watchman, tell me**
>
> **Watchman**, tell us of the night, What its signs of promise are. Traveller, o'er yon mountain's height See that glory beaming star. Watchman, does its beauteous ray Aught of joy or hope foretell? Traveller, yes; it brings the day, Promised day of Israel - Niambie, Ee **mlinzi**, Umepambazuka je! Utukufu wa Zayuni; Pana dalili zake? Msafiri uondoke, Utazame mbinguni, Kiunoni ujifunge, Ni kucha, alifajiri.
>
> **Watchmen, on the walls of zion**
>
> **Watchmen**, on the walls of Zion, What O tell us, of the night? Is the daystar now arising? Will the morn soon greet our sight? O'er your vision Shine there now some rays of light? O'er your vision Shine there now some rays of light? - Je! **Mlinzi**

ukutani wa mji wa Zayuni, Habari zake usiku? Asubuhi karibu? Kuna dalili za kupambazuka? Kuna dalili za kupambazuka?

**Hark! The voice of Jesus**

If you cannot be the **watchman**, Standing high on Zion's wall, Pointing out the path to heaven, Offering life and peace to all; With your prayers and with your bounties You can do what Heaven demands, You can be like faithful Aaron, Holding up the prophet's hands - Ingawa huwezi kuwa **Mkesha** mlangoni, Ukiwatolea watu Nafasi ya uzima; Kwa sala na kwa sadaka Watoa msaada, Kama Harun mwaminifu, Kuinua Mikono.

Nomino mlinzi, walinzi au mkesha katika lugha lengwa haijifungi na jinsia maalum kama ilivyo katika matini chanzi. Ulinganifu huu wa maana unatokana n azote mbili (Kiingereza na Kiswahili) kudhihirisha hali hii ya kutumia neno moja linalosimamia jinsia zote mbili.

**Men**

Nomino hii imetumika mara ishirini na sita katika matini chanzi. Katika matini lengwa, nomino hii inaashiria jinsia ya kiume katika hali ya kawaida. Hata hivyo katika muktadha wa lugha chanzi, nomino hii imetumika kurejelea jinsia zote mbili; jinsia ya kike na ya kiume. Tazama mifano ifuatayo:

**The church has one foundation**

Though with a scornful wonder **Men** see her sore oppressed, Though foes would rend asunder The Rock where she doth rest Yet saints their faith are keeping; Their cry goes up, "How long?" And soon the night of weeping Shall be the morn of song - **Watu** Hustaajabu Kwa Mashaka Yote Yaipatayo Nje Hata Ndani Mwote; Ila Watakatifu Humwomba, Wakikesha Usiku Ni Kilio, Asubuhi Raha.

**Hark! The voice of Jesus**

While the souls of **men** are dying, And the Master calls for you, Let none hear you idly saying, "There is nothing I can do!" Gladly take the task He gives you, Let His work your pleasure be; Answer quickly when He calleth, "Here am I, O Lord, send me." - Roho za **watu** zikifa, Bwana akikuita, Usiseme kwa uvivu, "Hakuna kazi kwangu." Kwa furaha anza kazi Ile aliyokupa, Ukajibu mara moja "nipo Bwana, nitume."

Nomino hii imetafsiriwa katika lugha lengwa kama watu. Tafsiri hii haiashirii jinsia maalum katika matini lengwa. Hapa mtafsiri ametumia tafsiri fasiri ili kufikia neno watu inayobeba dhana ya matini chanzi.

### 3.2 Jinsia ya Kisarufi

Jinsia ya kisarufi huainisha viumbe ambavyo kibayolojia haviwezi kuainishwa kama ni vya kike au kiume kwa kuvihusisha na jinsia fulani. Katika lugha mbili zinazohusika katika utafiti huu; Kiingereza na Kiswahili, lugha ya Kiingereza ndiyo inayodhihirisha jinsia ya kisarufi huku lugha ya Kiswahili ikikosa uainishaji huu wa kijinsia. Katika muktadha huu ambapo lugha chasili inadhihirisha jinsia ya kisarufi na lugha lengwa haina mfumo sawia wa kijinsia, tofauti za maana kati ya matini chasili na matini lengwa huweza kuibuka. Mifano hii inadhihirisha hali hiyo:

**Come we that Love the Lord**

We're marching to Zion, Beautiful, **beautiful Zion**; We're marching upward to Zion, The beautiful city of God. - Twenenda zayuni, **mji mzuri zayuni**! Twenenda juu zayuni, Ni maskani ya Mungu.

**Sing them over again**

Beautiful words, wonderful words, wonderful words of life. **Beautiful words**, wonderful words, wonderful words of life. - Maneno ya uzima ni **maneno mazuri**, Manemo ya uzima ni maneno mazuri.

Kivumishi beautiful huhusishwa Katika mifano yote (hapo juu), kivumishi "beautiful" katika matini chasili kimetumika kurejelea ubora au uzuri wa nomino mji (city) na maneno (words). Kwa msingi huu, tafsiri ya neno hili katika matini lengwa (mzuri na mazuri) imetumika ili kuafiki muktadha husika.

**Watch ye saints**

Nations wane, though proud and stately; Christ His kingdom hasteneth greatly; **Earth her latest pangs is summing**; Shout, ye saints, your Lord is coming. - Mataifa yapotea, **nchi zajaa uchungu**: Kristo anaharakisha, Unabii unatimizwa.

**Joy to the World**

Joy to the world, the Lord is come! **Let earth receive her King;** Let every heart prepare Him room, And heaven and nature sing, And heaven and nature sing, And

heaven, and heaven and nature sing. - Furaha kwa ulimwengu, **Bwana atakuja**! Kila moyo umpokee, Viumbe imbeni, Viumbe imbeni, Viumbe vyote imbeni.

Katika mifano huu, nomino kanisa (church) katika matini chasili imehusishwa na maneno yanayoashiria jinsia ya kike (her, she, bride). Katika matini lengwa, uashiriaji huu wa kijinsia haupo. Badala yake, vimilikishi visivyohusishwa na jinsia maalumu (-ake) ndivyo vimetumika huku baadhi ya dhana hizo za kijinsia zikidondoshwa katika matini lengwa. Hali hii hutokana na uhalisia kuwa lugha ya Kiswahili haina uashiriaji huu wa kijinsia. Hata hivyo, vipengele hivi vya jinsia ya kisarufi havichangii moja kwa moja katika tofauti za maana kati ya matini mbili husika.

Nomino nyingine zinazopewa jinsia katika Kiingereza ni pamoja na *church* (*her, she, bride*), lakini tafsiri ya Kiswahili haitoi uashiriaji huo wa kijinsia.

**4.0 Mahitimisho**

Utafiti huu ulitumikisha nadharia ya wingimifumo kuchunguza sababu za mwachano wa maana katika tafsiri za nyimbo kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili. Matapo mawili ya kijinsia yalichunguzwa yakiwemo jinsia ya kisemantiki na jinsia ya kisarufi. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa lugha ya Kiingereza ina uashiriaji mkubwa wa kijinsia kupitia vipengele mbalimbali vya kisarufi kama vile viwakilishi, nomino na hata virai. Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, isipokuwa katika nomino chache tu, lugha hii haina uashiriaji wa kijinsia kupitia kwa vipengee hivi vya kisarufi. Hivi ni kumaanisha kuwa, katika tafsiri zinazofanywa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili, jinsia ni suala mahusui la kitamaduni. Hii ni kwa sababu linapatikana katika lugha chanzi (Kiingereza) lakini linakosekana katika lugha lengwa (Kiswahili).

Utafiti huu vilevile umebaini kuwa jinsia ni kipengee muhimu katika uekezaji wa maana katika matini mbalimbali. Kwa msingi huu, ili pawe na ulinganifu wa maana kati ya matini chanzi (katika lugha Kiingereza) na matini lengwa (katika lugha ya Kiswahili) basi ni sharti pawe na uashiriaji sawa wa kijinsia katika ya lugha mbili husika. Hata hivyo, kwa sababu lugha ya Kiswahili inakosa uashiriaji huu wa kijinsia, maana katika matini chanzi na ile maana katika matini lengwa zinaishia kutofautiana. Kimsingi, utafiti huu umebaini kuwa jinsia ni mhimili mkubwa katika kuibua maana kwenye matini iliyoandikwa katika lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, inabainika wazi kuwa maana katika tafsiri za nyimbo kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili huweza kudhihirisha tofauti kwa sababu za kijinsia. Hii ni kwa sababu lugha hizi mbili husika zina mfumo tofauti wa kitamaduni wa kuashiria masuala mbalimbali ya kijinsia. Jambo hili hufanya maana inayoambatana na jinsia katika matini chasili kupotea katika matini lengwa.

**Marejeleo**

Aixelá, F. (1996). Culture-specific items in translation. In R. Álvarez & M. C. Vidal (Eds.), *Translation, power, subversion* (pp. 52–77). Clevedon: Multilingual Matters.

Ali, C. W. (1981). *The problems of translating from English into Swahili as exemplified by V.O.K. news items*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Baker, M. (1991). *In other words: A coursebook on Translation*. London: Routledge.

Even-Zohar, I. (1978). The Position of Translated Literature within the Literary Polysystem. In *Papers in Historical Poetics*. Tel Aviv: Porter Institute.

Gentzler, E. (1993). *Contemporary Translation Theories*. London: Routledge.

Gentzler, E. (2001). *Contemporary Translation Theories* (2nd ed.). Clevedon: Multilingual Matters.

Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Habwe, J., & Zaja, O. (2019). *Kamusi ya Isimu na Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kenya Review and Herald Publishers. (1985). *Adventist Hymnal*. Kendu Bay: Kenya Review and Herald Publishers.

Kenya Review and Herald Publishers. (1998). *Nyimbo za Kristo*. Kendu Bay: Kenya Review and Herald Publishers.

Kothari, C. R. (1985). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley.

Matei, A. (2014). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mugenda, O., & Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Mule, K. (2002). Translation, mistranslation, and cultural theory: African inflections, challenges, and prospects. *Metamorphoses*, *10*(1). Retrieved from https://www.smith.edu/metamorphoses/issues/2002spring.html

Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Applications*. London: Routledge.

Newmark, P. (1988). *A textbook of Translation*. New York: Prentice Hall.

Okiomeri, R. O. (2009). *Challenges of Translating English Hymns into Ekegusii: A case study of Adventist Church Hymnal* (Master's thesis). Kenyatta University.

Ondara, K. R. (2010). *Ufaafu wa Maana katika Tafsiri ya Nyimbo Dini.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Kenyatta

Ongati, A. R. (2004). *Text-Melody Relationships: Translation of European Hymns into Dholuo* Tasnifu ya Uzamili: Kenyatta University.

Stitt, R. (2016). *Linguistic Gender and Translation Studies*. Oxford: Oxford University Press.

Toury, G. (1980). The Nature and Role of Norms in Translation. In L. Venuti (Ed.), *The Translation Studies Reader* (pp. 200–218). Abingdon: Routledge. (2004 Edition)

Waihiga, G. (1999). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Zaja, O. (2006). *Siting Text, Culture, Context and Pedagogy in Literary Translation*. Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha Kenyatta

Zaja, O. (2021). *Utafiti na Uchanganuzi wa Fasihi Tafsiri ya Kiswahili*. Nairobi: Utafiti Foundation.